KAHAMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES (REG/HAS/171)
P.O.BOX 424, KAHAMA – SHINYANGA

Tel: +255 766 640 531,
+255 683 170 921

Tovuti: www.kachs.ac.tz ,
Barua pepe: admin@kachs.ac.tz,
admission@kachs.ac.tz,
info@kachs.ac.tz

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA CHUO

Kwa kuzingatia dhima na maono ya chuo, yaani; "*Kuandaa wahitimu wenye ujuzi na weledi wa hali ya juu katika tasnia ya afya*", chuo kwa sasa kinatoa mafunzo katika kozi zifuatazo:

(i) Technician Certificate in Pharmaceutical Sciences (Miaka 2);

(ii) Ordinary Diploma in Pharmaceutical Sciences (Miaka 3);

(iii) Technician Certificate in Clinical Medicine (Miaka 2); na

(iv) Ordinary Diploma in Clinical Medicine (Miaka 3).

MAHALI CHUO KILIPO.

Chuo cha Sayansi za Afya Kahama (KAHAMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES) kiko mkoani Shinyanga; umbali wa Kilometa 4 kutoka mjini Kahama. Unapowasili mjini Kahama kwa basi au usafiri mwingine wowote, unaweza kuchukua taxi au pikipiki za magurudumu matatu (bajaj) ziendazo **Mwendakulima** (mashariki mwa mji). Kabla ya kufika Mwendakulima, omba kushushwa Kahama College; chuo kiko pembezoni mwa barabara kuu ya Kahama - Shinyanga/Dar es salaam. Usafiri wa Bajaj unapatikana muda wote kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 1.00 usiku.

MAELEKEZO WAKATI WA KURIPOTI CHUONI

Mara baada ya kuwasili chuoni, wanafunzi wote wanapaswa kuripoti ofisi ya Msajili wa wanafunzi chuoni pamoja na ofisi ya malipo wakiwa na vitu vifuatavyo kwa ajili ya kusajiliwa:

(a) Barua ya kuchaguliwa kujiunga na Chuo cha Sayansi za Afya KAHAMA (Admission Letter).

(b) Fomu ya vipimo vya Afya (Medical Examination Form) iliyojazwa na daktari baada ya mwanafunzi kufanyiwa vipimo kikamilifu katika hospitali ya serikali. (Fomu kwa ajili ya vipimo vya afya zinapatikana katika tovuti ya chuo: (www.kachs.ac.tz).

(c) Cheti halisi cha Sekondari (au results slip kama muda wake haujaisha).

(d) Vitambulisho/Hati za kusafiria/Viza kwa wanafunzi watokao nje ya Tanzania.

(e) Nakala halisi (original) ya cheti cha kuzaliwa AU kiapo cha mahakama (Affidavit).

(f) Picha nne za paspoti zilizopigwa hivi karibuni.

(g) Karatasi ya benki (uthibitisho wa malipo) ya karo na gharama nyinginezo.

(h) Tsh 18000/= kwa ajili ya ream na glavs (examination gloves) -*mara moja kwa muhula.*

(i) Mashuka mawili na chandarua (mosquito net)

ANGALIZO: Ni makosa kisheria kutoa taarifa za uongo au kugushi, ikiwemo vyeti, stakabadhi ya malipo au nyaraka yoyote. Hatua za kisheria zaweza kuchukuliwa kwa atakayebainika kufanya hivyo.

KARO NA MICHANGO MINGINE

Karo italipwa, ama yote kwa mkupuo mmoja mwanzoni mwa mwaka wa masomo, au mikupuo miwili inayolingana; yaani mkupuo mmoja kila mwanzo wa muhula (Semester). Ada ikishalipwa, hairudishwi iwapo mwanafunzi ataamua kuondoka chuoni kwa utashi wake bila idhini ya mkuu wa chuo au iwapo atafukuzwa chuo kutokana na sababu za kitaaluma au za kinidhamu.

Hata hivyo, asilimia hamsini (50%) ya ada iliyolipwa yaweza kurudishwa iwapo mwanafunzi atatoa taarifa za kweli zinazomlazimu kuacha masomo, ndani ya majuma manne (wiki nne) tangu mwaka wa masomo kuanza.

Majedwali yafuatayo yanaonyesha kiasi cha ada na mpangilio wa ulipaji:

MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO MINGINE - FANI ZA UTABIBU

S/N	AINA YA MALIPO	KIASI (Tsh)		
		Muhula wa 1	**Muhula wa 2**	**JUMLA**
1.	Karo	900,000/=	900,000/=	1800,000/=
2.	Malazi	150,000/=	150,000/=	300,000/=
3.	**Kitambulisho****	**15,000/=**	**-**	**15,000/=**
4.	Umoja wa wanafuunzi	15,000/=	-	15,000/=
5.	Practical Procedure book & Practicum Guide	100,000/=	-	100,000/=
6.	Mitihani ya ndani	150,000/=	150,000/=	300,000/=
7.	TEHAMA	50,000/=	-	50,000/=
8.	Usajili	10,000/=	10,000/=	20,000/=
9.	Uhakiki ubora (NACTE Quality Assurance)	15,000/=	-	15,000/=
10.	Bima ya Afya*	60,000/=	-	60,000/=
11.	Mtihani wa Wizara****	150,000/=		150,000/=
12.	Mahafali***	10,000/=	-	10,000/=
TOTAL		**1,625,000/=**	**1,210,000/=**	**2,835,000/=**

*Wanafunzi wenye bima zao toka nyumbani, hawalazimiki kulipia bima ya Afya 60,000/=

**Gharama ya kitambulisho ni mara moja kwa kipindi chote cha masomo; isipokuwa mwanafunzi atakayepoteza au kuharibu kitambulisho, atalazimika kulipia gharama ya kupata kitambulisho kingine.

***Michango ya mahafali ni shilingi 10,000 /= kwa wanafunzi wanaoendelea na 50,000 /= kwa wanaohitimu.

****Ada ya Mtihani wa Wizara ilipwe kupitia Benki ya BOA

MAHITAJI MAALUMU KWA KOZI YA UTABIBU (CLINICAL MEDICINE)

Kila mwanafunzi katika kozi ya utabibu (cheti na diploma) anapaswa kuripoti chuoni na mahitaji yafuatayo kwa ajili ya kutumia katika masomo yake na katika mafunzo ya vitendo hospitalini:

1. Kipima Presha (Blood pressure machine) 1
2. Stethoscope (Litman) 1
3. Examination Torch 1

4. Tape Measure 1

5. Patella hummer 1

6. Kipimajoto (Thermometer) 1

7. Tuning fork 1

8. Boksi la glavs (Examination gloves) 1

Vifaa hivi vyote (isipokuwa glavs), vinapatikana chuoni kwa gharama ya shilingi **120,000/=** kwa watakaopenda.

kuvipata chuoni. Pia unaruhusiwa kununua popote pale ili mradi viwe ni halisi na vyenye kufaa

kwa matumizi lengwa.

MCHANGANUO WA KARO NA MICHANGO MINGINE -FANI YA FAMASI

S/No	ITEM	AMOUNT (TSH)		
		SEMENSTER 1	SEMESTER 2	Total
1	Karo	900,000/=	900,000/=	1,800,000=
2	Malazi	150,000/=	150,000/=	300,000/=
3	**Kitambulisho****	**15,000/=**	**-**	**15,000/=**
4	Umoja wa wanafunzi	15,000/=	-	15,000/=
5	Mitihani ya ndani	125,000/=	125,000/=	250,000/=
6	TEHAMA	50,000/=	-	50,000/=
7	Community Field work.	150,000/=	-	150,000/=
8	Usajili	10,000/=	10,000/=	20,000/=
9	Log book	50,000/=	-	50,000/=
10	Uhakiki ubora (NACTE Quality assurance)	15000/=	-	15,000/=
11	Bima ya Afya*	60,000/=	-	60,000/=
12	Mtihani wa Wizara****	150,000/=		150,000/=
13	Graduation***	10,000/=	-	10,000/=
TOTAL		**1,700,0000/=**	**1,185,000**	**2,885,000**

*Wanafunzi wenye bima zao toka nyumbani, hawalazimiki kulipia bima ya Afya 60,000/=

**Gharama ya kitambulisho ni mara moja kwa kipindi chote cha masomo; isipokuwa mwanafunzi atakayepoteza au kuharibu kitambulisho, atalazimika kulipia gharama ya kupata kitambulisho kingine.

***Michango ya mahafali ni shilingi 10,000 /= kwa wanafunzi wanaoendelea na 50,000 /= kwa wanaohitimu.

****Ada ya Mtihani wa Wizara ilipiwe Benk ya **BOA**

MAHITAJI MAALUMU -FANI YA FAMASI:

Wanafunzi wa fani ya Famasi pia wanatakiwa kuja na mahitaji yafuatayo:

1. Kikokotoleo (Scientific Calculator)
2. Glavs (Examination gloves) -1box @muhula
3. Bunda la karatasi (Ream) - 1 (@muhula

Njia ya kufanya malipo:

JINA LA AKAUNTI: KAHAMA COLLEGE OF HEALTH SCIENCES :

1. **CRDB -NAMBA YA AKAUNTI: 0150222187900.** –(Karo pekee)

2. NMB A/C No. 30610017310.(Michango mingine)
3. BANK OF AFRICA (BOA); - A/C No 05062970001 (Michango mingine)

Malipo kwa njia ya Cheki (Cheque) au “International Money Orders” yatapokelewa tu baada ya benki kukamilisha miamala husika.

Angalizo:

Usifanye malipo kwa M-PESA, TIGO PESA, AIRTEL MONEY au njia nyingine tofauti na akaunti za benki zilizotajwa hapo juu. Hatupokei pesa tasilimu.

SARE ZA CHUO:

Wanachuo wa kike:

- Magauni mawili (2) meupe yanayovuka magoti, yenye mikono mifupi na vifungo kifuani, kitambaa cha cotton (au chochote chenye 'material' mazito).

- Makoti mawili ya kitabibu (mikono mirefu).

- Viatu vyeusi na soksi nyeupe jozi (pea) mbili.

Wanachuo wa kiume:

- Suruali mbili za ***khaki*** zisizobana na za staha.

- Mashati mawili meupe ya mikono mifupi, kitambaa kizito.

- Makoti mawili meupe ya kitabibu (mikono mirefu).

- Viatu vyeusi na soksi nyeupe jozi (pea) mbili.

Sare zifuatazo hupatikana pia chuoni kwa bei zifuatazo:

- Suruali moja na shati moja (vyote) Tsh.**30,000/-,**
- Gauni moja Tsh.**30,000/=,**
- Koti la kitabibu (moja) Tsh. **30,000/=**

Mwanafunzi atakayeripoti chuoni na sare tofauti na zile zilizoelekezwa atalazimika kushona sare nyingine (upya).

MALAZI:

Chuo kinasisistiza wanafunzi wote kuishi chuoni (hosteli). Wanafunzi wote watakaa katika hosteli zilizoko maeneo ya chuo, isipokuwa kwa sababu zisizozuilika, ambapo mkuu wa chuo ataidhinisha baada ya kuzipima sababu na kuridhika; mfano mwanafunzi ambaye kwa sababu ya afya yake, anahitaji kuwa chini ya uangalizi wa wazazi wake siku kwa siku.

Wanachuo hawapikiwi chakula na chuo, isipokuwa chakula cha kununua kinapatikana katika mgahawa wachuo (Canteen) kwa bei nafuu. Gharama ya chakula kwa siku (milo mitatu) ni kati ya Sh. **3500/=** hadi **4000/=**

Muhimu:

1. KARO pekee italipwa kupitia benki ya CRDB. Malipo mengine yote yafanyike kupitia benki nyingine kama ilivyoainishwa hapo juu (**NMB** au **BOA**).

2. Vifaa vinavyotumia umeme kama vile heater, majiko ya umeme n.k., haviruhusiwi isipokuwa pasi ya kunyoshea nguo.

3. Vipengele vyote katika maelekezo haya ya kujiunga ni vya muhimu; unashauriwa kuvisoma vyote kwa umakini ili kuelewa na kutekeleza kwa usahihi mambo yaliyofafanuliwa.

****

MAWASILIANO:
Kwa maulizo yoyote, tafadhali wasiliana nasi kwa njia zifuatazo:
Phone +255766640531; +2555683170921
Whatsapp: +255756041312
E-mail: admission@kachs.ac.tz or admin@kachs.ac.tz